**Sera ya Ulinzi Salama wa Watoto na Vijana**

**Utangulizi**

Women Deliver[1] ni shirika kuu la kimataifa la kutetea usawa wa kijinsia na afya na haki za wasichana na wanawake; shirika hili linaamini katika haki asili, uhuru, utu, na ustawi wa watu wote. Shirika la Women Deliver linatetea ushiriki wa kimaana wa vijana kama waundaji-wenza na washirika katika kubuni programu na mikakati, kampeni, mipango ya utetezi na miundo ya kufanya maamuzi. Kipengele kikuu cha mtazamo huu ni kubadilisha fikra na mikakati kutoka kutekeleza programu *kwa* ajili ya vijana kuelekea hatua ya kukuza sauti zao na kufanya kazi *na* vijana ili kuunga mkono kazi yao ya utetezi kwa niaba ya wasichana, vijana, na wanawake, katika utambulisho wao wote unaoingiliana. Katika kazi hii yote, shirika la Women Deliver limejitolea kupunguza hatari ya unyanyasaji, dhuluma, unyonyaji, na aina nyingine za madhara ambayo vijana wanaweza kuathiriwa nayo wanapotafiti, kutetea, kutekeleza, na kuchangisha fedha kwa ushirikiano wa pamoja na wengine wanaofanya kazi kama hii. Women Deliver inaelewa kuwa ina wajibu wa kutayarisha na kutekeleza sera zinazolinda afya, usalama na ustawi wa watoto na vijana. Aidha, Women Deliver inaamini kwamba watu wazima walio katika nafasi za uongozi na uhusiano wa kuaminiana kwa watoto na vijana lazima watumie viwango vya juu zaidi vya uadilifu, uchunguzi unaostahili, na kupunguza hatari.

Ili kuunga mkono na kutekeleza ahadi hizi, Women Deliver hudumisha sera ya ulinzi salama inayohusiana na mahusiano kati ya na miongoni mwa wafanyakazi, washauri, wafanyakazi wa kujitolea na washirika ("Wadau") wa Women Deliver na watoto na vijana. Sera hii inawiana na Kifungu cha 19 cha **Mkataba** wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto, ambacho kinasisitiza haki ya watoto kulindwa dhidi ya "aina zote za unyanyasaji wa kimwili au kiakili, jeraha au dhuluma, kutelekezwa au kutoshughulikiwa ifaavyo, unyanyasaji au unyonyaji, ukijumuisha unyanyasaji wa kingono." Sera hii pia inaonyesha haki ya kila mtu kushughulikiwa kwa usawa, kiutu na kwa usalama kama ilivyobainishwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinadamu.

**Taarifa ya Sera**

Shirika la Women Deliver halikubali kamwe unyanyasaji wa kimwili, kihisia, kingono, na wa mtandaoni, unyonyaji, kutelekezwa, au kuwadhuru watoto (mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18) au vijana (mtu yeyote aliye kati ya umri wa 18-29) katika Programu za Women Deliver (tazama ufafanuzi).

Women Deliver inalenga kuzuia unyanyasaji wowote, unyonyaji, madhara, au kupuuzwa kwa kuimarish ulinzi salama katika muundo wa programu zake na kuchukua mtazamo wa "Usidhuru" (kama inavyofafanuliwa chini ya Taarifa ya Kanuni). Tukio lolote ambalo linaweza kujumuisha ukiukaji wa Sera hii lazima liripotiwe mara moja kwa Mtu Aliyeteuliwa kwa mujibu wa Miongozo ya Utekelezaji wa Sera ya Ulinzi Salama wa Watoto na Vijana ya Women Deliver anayewajibikia ripoti zote, au Mdau yeyote wa Women Deliver aliye huru naye na ambaye si mhusika wa tukio. Kwa kujibu ripoti kama hizo, Women Deliver itachukua hatua ya kuhakikisha usalama wa haraka wa mtoto au kijana, na kuwasaidia katika kupata rasilimali zinazopatikana ambazo wanaweza kuzihitaji. Kisha Women Deliver itachukua hatua

[1]Women Deliver ni shirika lisilo la faida la 501(c)(3) linalopatikana nchini Marekani. Uidhinishaji wa Sera ya Ulinzi Salama wa Watoto na Vijana/Tarehe ya Kuanza Kutumika: Juni 1,2019; Ilifanyiwa Mapitio Novemba 2022.

kujibu ripoti kadri inavyofaa kutokana na ukali wa ripoti hiyo. Ripoti zote za unyanyasaji zitachunguzwa kwa kina. Ukiukaji wa Sera hii hautaruhusiwa na unaweza kusababisha taratibu za kinidhamu, kusitishwa kwa kazi au uhusiano, na uwezekano wa kushtakiwa kisheria.

Sera hii inatumika kwa Wadau wa Women Deliver, watoto na vijana, kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

**Taarifa za Kanuni**

Utekelezaji wa Sera hii unaongozwa na kanuni zifuatazo:

- Kuhakikisha afya na ustawi wa watoto na vijana ndio msingi wa Sera hii na ndiyo kanuni muhimu inayoendesha utekelezaji wa Sera hii. Hii inajumuisha kudumisha usiri wa utambulisho wa mtoto(watoto) na/au vijana waliohusika katika tukio hilo, pamoja na mzazi/mlezi wao, kadri inavyowezekana chini ya miktadha hiyo.
- "Usidhuru" inajumuisha kiwango cha juu zaidi cha kujitolea cha Women Deliver kwa vijana ambao hukutana nao kupitia kipindi cha kazi ya Women Deliver. Hii inajumuisha, na lakini sio tu, madhara ambayo yanaweza kutokea kupitia ushiriki wao katika programu zinazohusiana na Women Deliver, matukio, mawasiliano, kama sehemu ya uchangishaji fedha au kampeni ya mitandao ya kijamii, au katika jukumu la mashauriano.
- Wadau wa Women Deliver lazima waheshimu watoto na vijana, bila kujali rangi, utambulisho wa jinsia, utambulisho wa lugha, dini, maoni, uraia, kabila, wenye ulemavu, tabaka, mwelekeo wa kimapenzi au hali nyingine. Wanapaswa kuwashughulikia watoto na vijana ambao wanashirikiana nao kwa utaalamu na kufuata sheria husika kuhusiana na kufanya kazi na watoto na vijana. Wanapaswa kuzingatia hatari ya madhara wanapohusika au kufanya shughuli na watoto na vijana ikiwa kuna uwezekano wowote kwamba mtoto au kijana anaweza kudhulumiwa au kutumiwa vibaya kupitia ushiriki wao na Wadau wa Women Deliver.
- Watu hukumbana na hatari tofauti zinazohusiana na usalama wao wa kimwili, kiakili, na kihisia. Hatari hizi zinaweza kutofautiana kutokana na mambo yanayohusiana na utambulisho, hali, au sababu nyinginezo. Wakati sababu hizi zinapopishana, unaweza kuongeza uwezo wa mtoto au kijana kudhurika na madhara au hatari ya madhara. Mtazamo wa Women Deliver kuhusu ulinzi salama unatambua asili na kiwango tofauti cha hatari kinachotokana na sababu hizi.
- Watoto na vijana wanapaswa kupewa fursa yenye maana na sahihi ya kuchukua jukumu la kushiriki kikamilifu katika sera, shughuli, na maamuzi yanayowahusu na kuwahusisha. Wadau wa Women Deliver wanapaswa kuwa na njia za kuwafikia vijana na wale wanaowatetea/kuwawakilisha ili kuwasilisha wasiwasi wao, na wanapaswa kuzingatia kwa umakini na, ikiwezekana, kuchukua hatua kuhusu wasiwasi huo. Women Deliver itatoa ushauri kwa watoto na vijana wanaohusika katika programu zinazodhaminiwa na Women Deliver kuhusu uwepo wa Sera hii na kutarajia waizingatie, kwa njia inayolingana na umri wao. Ulinzi wenye ufanisi unahitaji kutumia kwa kawaida hatua za kupunguza hatari na hatua za haraka na kali kwa kulinda mtoto au kijana wakati tukio linaporipotiwa au linapotajwa.
- Mbinu ya ulinzi ya Women Deliver imejumuishwa katika vipengele vyote vya operesheni za Women Deliver, programu, miradi, matukio, mawasiliano, na ushirikiano.

**Upeo wa Matumizi**

Sera hii inatumika kwa Wadau wote wa Women Deliver kama ilivyoelezwa hapa, katika nchi zote ambapo Women Deliver inaendesha shughuli, iwe wakati wa saa za kazi au nje ya saa za kawaida za biashara. Ikizingatiwa kwamba Wakati Women Deliver itachukua tahadhari na jitihada za kudhibiti na kupunguza hatari kwa kiwango cha kutosha, kuna mipaka fulani inayotumika katika hali ambapo Women Deliver ina ushiriki finyu au udhibiti finyu wa mahusiano. Ikizingatiwa kwamba Women Deliver haitachukua jukumu katika hali kama hizo, shirika litatoa mwongozo na mapendekezo kama inavyofaa kwa lengo la kupunguza hatari ya madhara na kuboresha usalama.

**Ufafanuzi**

- **Unyanyasaji:** Mfululizo wa tabia zinazosababisha madhara halisi au yanayowezekana kwa afya, ustawi, uhai, ukuaji, au heshima kwa mtoto au kijana. Inajumuisha kitendo chochote au kushindwa kutenda ambako husababisha au kuleta hatari ya kifo au madhara makubwa yanayoweza kutokea. Matendo kama hayo yanaweza kuchukuliwa kama unyanyasaji bila kujali kama yana nia ya kusababisha jeraha. Unyanyasaji unaweza kuwa wa kihisia, mtandaoni, kimwili, au kingono:
    - **Unyanyasaji kiuchumi:** kitendo chochote kinacholenga kudhibiti rasilimali za kiuchumi za mtoto au kijana, kupunguza mamlaka ya mtoto au kijana juu ya ustawi wao wa kiuchumi, au vinginevyo kutumia vibaya mtoto au kijana kwa faida za kiuchumi.
    - **Unyanyasaji kihisia:** Matendo au kutokutenda ambako kunasababisha majeraha kwa uwezo wa kisaikolojia au utulivu wa kihisia wa mtoto au kijana. Unaweza kujumuisha uonevu, unyanyasaji, kudhalilisha, kuaibisha, kudhibiti au kulaumu kwa njia isiyofaa, kumkosea heshima, kumdhalilisha, au kumdharau, na shughuli zozote zile ambazo zinamfanya mtoto au kijana ajisikie kutengwa, kudunishwa, au kuaibishwa.
    - **Unyanyasaji Mtandaoni:** Aina yoyote ya unyanyasaji unaotokea kwenye mtandao, ikiwemo kupitia kompyuta, tableti, na simu za mkononi, na unafanyika katika nafasi yoyote mtandaoni, ikijumuisha mitandao ya kijamii, jumbe na programu za ujumbe, baruapepe, mazungumzo ya mtandaoni, michezo ya mtandaoni, au tovuti za utangazaji moja kwa moja. Unyanyasaji au dhuluma mtandaoni ni pale ambapo mtu au kikundi cha watu wanaunda mazingira yenye uhasama ambayo yanamdhalilisha, kumnyanyasa, kumtisha au kumnyamazisha mtu binafsi[2].
    - **Unyanyasaji kimwili:** Matumizi ya nguvu na mtu yeyote kwa sehemu yoyote ya mwili ambayo husababisha madhara halisi au yanayowezekana, jeraha, au mateso (ambayo siyo lazima yawe dhahiri). Unyanyasaji wa kimwili unaweza kujumuisha kutikisa, kupiga ngumi, kunyonga, kung'ata, kupiga teke, kuteketeza, kupiga, kutupa, kutia sumu, au kushikilia chini ya maji.
    - **Unyanyasaji wa kingono:** Unyanyasaji halisi au jaribio la unyanyasaji katika hali ya udhaifu, nguvu tofauti, au imani kwa madhumuni ya kingono. Hii inajumuisha kulazimisha, kushinikiza, au kushawishi mtoto au kijana kushiriki katika aina yoyote ya vitendo vya ngono, kama vile kupenya kwenye sehemu za siri, ubakaji, ngono ya mdomo, kuguswa au kufichuliwa kwa njia ya kuaibisha, kutumia lugha ya ngono wazi au

[2]"Mwongozo wa Kulinda Usalama Mtandaoni kwa Viongozi wa Wasichana na Vijana wa AGIP," Mpango wa Uwekezaji kwa Wasichana Wadogo, Plan International, na Girls Not Brides." 2021.

ya uchochezi kwa mtoto au kijana, ukatili au kujihusisha na tabia inayohusisha kugusana kimwili na ambayo nia yake inachochea ngono, au kumwonyesha mtoto au kijana picha za ngono. Aina zote za unyanyasaji wa kingono na ukatili wa kingono, ikiwemo ngono na jamaa wa ukoo, ndoa za mapema na lazima, ukahaba ulio lazimishwa, ukeketaji au kukata sehemu za siri za wanawake, na utumwa wa kingono, zinachukuliwa kama unyanyasaji wa kingono. Kutumia matamshi ya ngono, mizaha, udaku au kejeli kuhusu mwili wa mtoto au kijana au mwelekeo wa kingono au kuoa

Mialiko, maombi au maoni ya kingono yanayohusiana na kujishughulisha, kuridhisha, faida na masilahi binafsi ya Mdau wa Women Deliver ambaye yuko katika nafasi ya uaminifu au mamlaka na ambaye mtoto au kijana ana uhusiano wa kutegemea unakatazwa kabisa.

- **Watoto:** Mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18, kama ilivyoelezwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto. Ufafanuzi wa mtoto kwa madhumuni ya Sera hii usihitilafiane na ufafanuzi wa kisheria wa mtoto au kikomo cha umri kilichowekwa katika sheria nyingine husika. Ukweli kwamba kijana chini ya umri wa miaka 18 anaweza kuwa amefikia umri wa kuridhia ngono, umri wa kupiga kura, au hatua nyingine ya umri inayohusiana haubadilishi hatari yake kama mtoto.
- **Unyonyaji:** Hali yoyote ambapo mnyanyasaji anatumia uwezo wake wa nguvu na/au hadhi ya kiuchumi isiyo sawa ya mtoto au kijana kwa faida ya kifedha, kazi, kuridhika kingono, au aina nyingine ya faida ya kibinafsi au kifedha.
- **Madhara:** Athari mabaya kwenye ustawi wa kimwili, kisaikolojia, au kihisia wa mtoto au kijana. Madhara yanaweza kusababishwa na unyanyasaji, kutelekezwa au unyonyaji, iwe kimaksudi au kwa bahati mbaya, na pia yanaweza kusababishwa na mtoto au kijana mwenyewe ("kujidhuru").[3]
- **Kutelekezwa:** Kutotimiza mahitaji ya msingi ya kimwili na/au kisaikolojia ya mtoto au kijana ambako husababisha madhara halisi au yanayowezekana kwa afya, ustawi, uhai, ukuaji, au heshima ya mtoto au kijana. Kunajumuisha kuchukua hatua ambazo hazimlindi mtoto au kijana kutoka kwa hatari au hatua ambazo zinaweza kumweka mtoto au kijana katika hatari kubwa ya unyanyasaji au unyonyaji.
- **Wadau wa Women Deliver:** Wanafafanuliwa kama wafanyakazi wa Women Deliver (wa kudumu au wa muda mfupi) na mtu yeyote mwingine anayehusika katika shughuli za Women Deliver, ikijumuisha wanagenzi, washauri, wanakandarasi, wafanyakazi wa kujitolea, washirika, wabia, watafiti, vyombo vya habari, wajumbe wa Bodi na maafisa, washiriki wa Programu ya Viongozi Vijana, wahitimu wa Programu ya Viongozi Vijana, na vijana wengine wanaoshiriki katika shughuli za Women Deliver.
- **Vijana:** Mtu yeyote mwenye umri kati ya miaka 18-29.

**Ukaguzi wa Sera**

[3]Kumbuka: katika visa ambapo inaripotiwa au kugundulika kuwa mtoto au kijana anajidhuru, watapatiwa rufaa kwa rasilimali husika za msaada na hawataadhibiwa au kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa kitendo kama hicho.

Women Deliver itakagua na kusasisha Sera hii angalau mara moja kila baada ya miaka mitatu, au mara nyingi zaidi ikiwa kutakuwa na mabadiliko makubwa katika muktadha, teknolojia au wigo wa kazi za Women Deliver, ili iwe sawa na maendeleo ya kisheria, ya shirika, na ya programu.